## 3.0 WAJIBU WA TAASISI MBALIMBALI ZA SERIKALI KWENYE UKUSANYAJI WA ADA YA HUDUMA ZA UMWAGILIAJI

**3.1 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji.**

- Kutoa hati ya madai (invoice) kwa muda uliopangwa kwa vyama vya wakulima wamwagiliaji.
- Kutoa namba maalumu ya malipo (Control number) kwa vyama vya wakulima wamwagiliaji.
- Kufanya ukaguzi wa ukusanyaji wa Ada ya Huduma za Umwagiliaji kwa mujibu wa sheria.
- Kutoa risiti ya kieletroniki kwa malipo yaliyofanyika ndani ya siku tano za kazi baada ya malipo kupokelewa kwenye akaunti ya Tume.
- Kuhakikisha risiti ya malipo ya kieletroniki iliyotolewa na Tume imepokelewa na vyama vya wakulima wamwagiliaji.

**3.2 Wajibu wa Serikali za mitaa katika ukusanyaji wa Ada ya Huduma za Umwagiliaji**

- Kuhakikisha malipo ya Ada za Huduma ya Umwagiliaji kutoka vyama vya wakulima wamwagiliaji yanapelekwa Tume kupitia namba maalumu ya malipo (Control Number) ilitolewa na Tume kabla ya kuidhinishwa kwa matumizi mengine;
- Kutoa orodha ya vyama vya wakulima wamwagiliaji vilivyolipa kulingana na makato yaliofanyika; na
- Kuchukua hatua zozote za kisheria zitakazo hakikisha ulipwaji wa Ada ya Huduma za Umwagiliaji kufanyika kwa wakati

**3.3 Wajibu wa vyama vya wakulima wamwagiliaji katika Ukusanyaji wa Ada ya Huduma za Umwagiliaji**

- Kukusanya Ada ya Huduma za Umwagiliaji kwa mujibu wa sheria na kuziwasilisha Tume ya Taifa ya Umwagiliaji;
- Kuruhusu afisa aliyepewa dhamana na Tume kukagua na kulinganisha kiasi cha mavuno (volume of harvest) katika msimu husika;
- Kutunza kumbukumbu za daftari la wanachama katika uzalishaji wa mazao na kuboresha kulingana na taratibu;
- Kutoa taarifa sahihi za uzalishaji wa mazao kwa kila msimu;
- Kutoa risiti kwa wanachama waliolipa Ada ya Huduma za Umwagiliaji;
- kugharamia gharama zote zitazojitokeza katika ukusanyaji wa Ada ya Huduma za Umwagiliaji.

## 4.0 HITIMISHO

- Ni wajibu wa kila mkulima anayejihusisha na kilimo cha umwagiliaji kulipa Ada ya Huduma za Umwagiliaji kama ilivyoainishwa katika sheria ya Umwagiliaji kifungu 39 na kanuni ya 84 kwa uendelevu wa miundombinu ya Umwagiliaji
- Aidha kwa mujibu wa sheria na kanununi ya 85 na 105 mkulima anayejihusisha na kilimo cha umwagiliaji endapo atashindwa kulipa Ada ya Huduma za Umwagiliaji, anaweza kutiwa hatiani kwa kulipa faini isiyopungua Tshs 1,000,000/= au kifungo cha mwaka mmoja au vyote kwa pamoja

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:**
**TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI**
**S.L.P. 146, Njedengwa, Dodoma**
**Simu:** +255 26 296 2073
**Barua Pepe:** info@nirc.go.tz
**Facebook/Instagram/Twitter:** Nirc_tz
**Youtube:** Tume ya Taifa ya Umwagliaji
**Tovuti:** www.nirc.go.tz

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI**



# ADA YA HUDUMA ZA UMWAGILIAJI

## 1.0 UTANGULIZI

Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeanzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 3 (1) na (2) cha Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji Na 4 ya mwaka 2013, ikiwa na majukumu ya kuratibu, kuendeleza na kusimamia Kilimo cha Umwagiliaji. Pamoja na majukumu hayo Tume pia ina wajibu wa;-

- Kuhakikisha wakulima wote wanaomiliki ardhi kwenye skimu ya umwagiliaji wanakuwa wanachama wa vyama vya wakulima wamwagiliaji;
- Kuwajengea uwezo wakulima juu ya teknolojia za umwagiliaji katika skimu;
- Kujenga uwezo na Kuimarisha vyama vya wakulima wamwagiliaji;
- Kuhamasisha wakulima kuchangia Ada ya Huduma za Umwagiliaji; na
- Kuwezesha ubia kati ya sekta binafsi na ya umma kwa ajili ya uendeshaji na matunzo bora ya skimu za wakulima wamwagiliaji.



## 2.0 ADA YA HUDUMA ZA UMWAGILIAJI

Ada ya Huduma za Umwagiliaji ni Ada inayotakiwa kulipwa na wakulima katika vyama vya wakulima wamwagiliaji ambapo kila mkulima mwenye shamba katika eneo la skimu ya umwagiliaji atawajibika kuchangia 5% ya wastani wa mavuno kwa ekari kwa msimu.

Vyama vya wakulima wamwagiliaji vina wajibu wa kukusanya Ada hii kutoka kwa mkulima mmoja mmoja kama inavyoelekezwa katika kifungu cha 84 (1) cha kanuni za umwagiliaji za mwaka 2015. Kutochangiwa kwa Ada ya Huduma za Umwagiliaji kutoka kwa vyama vya wakulima wamwagiliaji ni kosa kisheria kama inavyofafanuliwa kwenye kanuni za umwagiliaji kifungu cha 105 cha mwaka 2015.

### 2.1 Taratibu za Ukusanyaji wa Huduma za Umwagiliaji

Mkulima atatakiwa kuchangia 5% ya wastani wa mavuno kwa ekari kwa msimu na kupeleka kwenye akaunti ya chama cha wakulima wamwagiliaji kwa skimu husika. Chama cha wakulima wamwagiliaji kitalipa Ada hiyo kwenye mfuko wa maendeleo ya umwagiliaji kupitia namba ya malipo itakayotolewa (Control number).

### 2.2 Umuhimu wa Ada ya Huduma za Umwagiliaji

Kwa upande wa vyama vya wakulima wamwagiliaji fedha za Ada ya Huduma za Umwagiliaji hutumika katika:-

- Kusaidia vyama vya wakulima wamwagiliaji kuweza kumudu gharama za uendeshaji na matunzo ya miundombinu ya umwagiliaji ikiwa ni kufanya shughuli za ukarabati mdogo kama vile; kupaka vilainishi kwenye mageti ya banio, kupaka rangi kwenye mageti na kuziba nyufa kwenye mifereji kwa wakati pale tatizo linapojitokeza;
- Uendeshaji wa ofisi za vyama vya wakulima wamwagiliaji;
- Kulipa watendaji wa ofisi za vyama vya wakulima wamwagiliaji; na
- Kugharamia shughuli zozote zitazojitokeza.

**Kwa upande wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Ada ya Huduma za Umwagiliaji hutumika katika:-**

- Kuongeza/kuendeleza eneo la kilimo cha umwagiliaji nchini ili uzalishaji wa chakula hasa kipindi hiki ambapo dunia inakabiliwa na changamoto ya mabadiliko ya tabia nchi ambayo yamepelekea kupungua kwa kiwango cha mvua duniani na mtawanyiko usio tabirika;na
- Kufanya ukarabati wa miundombinu kwa wakati pale uharibifu mkubwa wa miundombinu unapotokea ambao upo juu ya uwezo wa vyama vya wakulima wamwagiliaji.

